BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU UTEKELEZAJI WA USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA WIZARA YA UJENZI MAWASILIANO NA UCHUKUZI

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia afya njema na tukaweza kukutana hapa leo hii, ili kuendelea na shughuli zetu za kuwatumikia wananchi wetu. Aidha napenda kukushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuwasilisha Maoni ya Kamati Kuhusiana na utekelezaji wa Ushauri na maagizo ya Kamati yetu kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati yetu kwa mashirikiano makubwa katika kazi zetu za Kamati na hatimae tukaweza kuwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza letu tukufu, na kwa ruhusa yako naomba niwataje kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Yahya Rashid Abdulla(Mamba) - Mwenyekiti
2. Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Mjumbe
4. Mhe. Mussa Foum Mussa - Mjumbe
5. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe - Mjumbe
6. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
7. Ndg. Rahma Kombo Mgeni - Katibu
8. Ndg. Himid Haji Choko - Katibu

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu pamoja na kuridhika na hatua ya Wizara kwa kuongeza bajeti na vitendea kazi kwa Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Pia tunapongeza hatua za kuifanyia ukarabati Ofisi ya Mamlaka huko Pemba kwa kuzifanyia matengenezo ofisi zake ili kuimarisha mazingira bora ya kazi.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusiana na suala la leseni za Madereva, Kamati yetu inakubaliana na Uwamuzi wa Mamlaka wa kufuata miongozo ya Kimataifa na ya Kikanda ili hatimae kupata madereva mahiri kwa ajili ya usalama wa watumiaji wote wa barabara na pia kukidhi sifa katika soko la ajira kwa madereva wetu. Pamoja na hatua hiyo, Kamati inazidi kuishauri Wizara kuangalia uwezekano wa kufawafanyia majaribio madereva wanafunzi kwa kutumia gari za "**Automatic**" kulingana na uhalisia wa gari zinazotumika kwa wakati wa sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu kwa mara kadhaa imekuwa ikipokea malalamiko kuhusiana na taasisi mbali mbali kuharibiana miundombinu wakati wakifanya shughuli zao tofauti. Miongoni mwa taasisi hizo ni Mamlaka ya Usafiri Barabarani, Mkongo wa Taifa, ZAWA na ZECO. Kwa kuwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiiano na Uchukuzi imekiri kuunda Kamati ya wataalamu inayohusisha taasisi zinazoguswa na miradi ya barabara, tunaamini kwa sasa malalamiko ya kuharibiana miundo mbinu itamalizika na kufanya kazi kwa mashirikiano mazuri zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa maeneo tuliyoyaguswa katika maagizo ya Kamati, ni Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Uzi- Nga"mbwa, Kamati inahimiza kuharakishwa kwa michakato ya Mradi huo ili uanze kutekelezwa kwani hadithi zake zimekuwa za muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu imeshtushwa na harufu ya upotevu wa fedha za mapato ya Shirika la Bandari Tawi la Pemba kama ripoti ya Mheshimiwa Waziri inavyoonesha. Tunaishauri wizara kuwa makini na watendaji wake wanaohusika na mapato huku ikichukuwa hatua zinazofaa kwa wafanyakazi wake wachache wasiokuwa waaminifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inakubaliana na Uwamuzi wa Wizara wa kuuza meli zake za MV Maendeleo na MT Ukombozi zilizokuwa zikiendeshwa kwa hasara. Kadhalika, Kamati inaishauri Wizara kuwa makini na kufanya utafiti wa kutosha katika Matengenezo yake ya MV Mapinduzi II ambayo imekosa soko na kushindwa kuuzika. Pamoja na jitihada za kuifufua Meli hiyo, bado Kamati inasisitiza kwa Serikali kutafuta

usafiri wake wenyewe wa majini, kulingana na maumbile ya visiwa vya Unguja na Pemba na badala ya kutegemea vyombo vya watu binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Kamati yangu iliaagiza utafutaji wa hati miliki za maeneo yote Mamlaka Pemba na Unguja kwa lengo la kuyatambua na kuepusha uvamizi. Tunashukuru na kuridhika na utekelezaji wa Agizo hili. Hata hivyo Kamati inasikitishwa na tabia iliyojitokeza hivi sasa katika Uwanja wa Abeid Amani Karume Kisauni hasa maeneo ya pembezoni mwa Mlango Mkuu wa Abiria. Katika maeneo hayo tumekuwa tukishuhudia magari mengi ya abiria na ya kubebea wageni yamekuwa yakiegeshwa katika eneo hilo na kutoa taswira mbaya ya muonekano wake. Kamati inashauri Mamlaka kutafuta namna ya kuyadhibidi magari hayo kwa kuyaingiza katika maeneo ya maegesho ya magari ndani ya uzio wa Mamlaka hata kwa kiwango kidogo cha malipo.

**Mheshimiwa Spika,** nimalizie hotuba yangu kwa kukushukuru tena kwa kunipa fursa ya kuzungumza mbele ya Baraza lako tukufu na pia nawashukuru Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza kwa umakini na kwa utulivu mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ahsante na naomba kuwasilisha.



………………………

**(Mhe: Kombo Mwinyi Shehe)**
**Kny: Mwenyekiti,**
**Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**